## Maswali

1. Mungu alichagua nani kuwa nabii?
2. Mungu alisema nini itafanyika ikiwa watu hawatatubu?
3. Nani aliandika kwa chuo maneno yenye Yeremia alisema?
4. Mfalme muovu Yehoyakimu alifanyaje chuo?
5. Yeremia na Baruku walifanya nini baada ya chuo kuharibiwa?
6. Nini ilifanyika kwa Mfalme Yehoyakimu?
7. Makuhani na wakuu walifanyaje Yeremia alipoleta ujumbe kutoka kwa Mungu?
8. Nani alimwokoa Yeremia? Alimwokoa namna gani?
9. Nini ilifanyika kwa Mfalme Sedekia wakati Yerusalemu ilichukuliwa?
10. Nini ilifanyika kwa Yeremia? Nini ilifanyika kwa Ebedmeleki?

## Majibu

1. Mungu alichagua Yeremia kuwa nabii.
2. Wababeli wangekuja na waiharibu nchi.
3. Baruku aliandika maneno ya Mungu kwa chuo.
4. Mfalme alikata chuo kwa kijembe na kuichoma.
5. Kwa siri Yeremia na Baruku waliandika hayo maneno tena kwa chuo ingine.
6. Mfalme Yehoyakimu alichukuliwa mateka hati Babeli.
7. Walitupa Yeremia kwa kisima na akagwama kwa matope.
8. Ebedmeleki aliokoa Yeremia. Alimvuta kwa kamba.
9. Mfalme Sedekia alichukuliwa. Wana wake waliuawa. Walimpofusha na kupelekwa Babeli.
10. Yeremia alikubaliwa kubaki kwa nchi yake. Ebedmeleki aliokolewa.



# 79 Yeremia

### Kwa Biblia

Yeremia 36:1 – 8; 19 – 23 na Yeremia 38:1 – 13

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Yeremia alitii Mungu hata kama maisha yake yalikuwa hatarini. Alijaribu kuponya watu wake kutoka kwa Wababeli. Mungu hulinda wale wanaomtegemea

### Somo

Yeremia alipokuwa bado mtoto, Mungu alimwambia kwamba alikuwa amemchagua kuwa nabii wa Yuda. Nabii ni mtu anayeadharisha watu na kuwapea moyo. Aliambia watu maneno ya Mungu. Tena nabii angeambia watu yanayokuja kufanyika baadaye.

Wakati wa mfalme mzuri kama Yosia, nabii Yeremia alipea watu moyo na kuwasaidia. Baada ya Yosia kufa, wafalme waliofuata walikuwa waovu. Watu waliaja Mungu tena. Kazi ya Yeremia ilikuwa ngumu sana kwa sababu watu hawakutaka kusikia maneno ya Mungu. Walimcheka Yeremia tena walikuwa wakimteza.

Yeremia aliambia watu kwamba walitakiwa watubu na wasikilize ujumbe wa Mungu. Yeremia alihadharisha watu wa Yuda kwamba wasipotii Mungu, Wababeli watakuja kuwashambulia. Nchi yao itaharibiwa. Yeremia alihuzunika sana alipoona Wababeli wanajitayarisha kuja kuwashambulia. Lakini watu hawakutaka kusikia ujumbe wa Mungu ulioletwa na Yeremia.

Mfalme Yehoyakimu alikuwa mwana wa Mfalme mzuri Yosia. Lakini alikuwa mfalme mbaya sana.

Mungu aliambia Yeremia aandike chini hadhari zote alizokuwa ameambia watu wake. Tena alimwambia aandike chini uovu wote wenye walifanya. Yeremia alichukua chuo. Alisema maneno yote yenye Mungu alimwambia. Baruku mwandishi aliandika kwa chuo maneno ya Yeremia yote. Chuo ilipelekewa Mfalme Yehoyakimu.

Mfalme Yehoyakimu alikuwa amekaa karibu na moto kwa nyumba aliyokaa wakati wa baridi. Walimsomea chuo. Mfalme Yehoyakimu alikasirika sana aliposikia hadhari ya Mungu kwamba Wababeli watakuja kuharibu ufalme wa Yuda. Alikasirika kwa sababu Mungu alisema yeye alifanya mambo maovu. Mfalme Yehoyakimu alikata kwa kijembe kila ukurasa uliosomwa. Alitupa vipande vya chuo motoni. Vilichomeka mpaka vikawa jivu.



Mfalme Yehoyakimu alirarua na kuchoma chuo. Lakini haingewezekana kuharibu maneno ya Mungu. Mungu aliambia Yeremia na Baruku kuandika chuo ingine tena. Waliandika kwa siri tena maneno ya Mungu yote kwa chuo ingine.

Maneno ya Mungu yaliyokuwa kwa chuo ni ya kweli. Baada ya miaka michache, Nebukadreza mfalme wa Babeli alishambulia Yuda. Nabukadreza alichukua Yehoyakimu Mfalme muovu mateka. Nebukadreza alimfanya Sedekia mfalme wa Yuda. Ilimbidi Sedekia atii Nebukadreza.

Mungu alipea Yeremia ujumbe tena. Yeremia aliambia Mfalme Sedekia, makuhani na wakuu huo wote ujumbe wa Mungu. Mungu aliwambia wamtii Mfalme Nebukadreza. Wakimtii Mfalme Nebukadreza, watakaa kwa nchi yao kwa amani. Lakini wakiasi Mfalme Nebukadreza, Mungu alisema, watashindwa na kuchukuliwa mateka mpaka Babeli. Mfalme Sedekia, makuhani na wakuu wote hawakusikiliza Yeremia. Walikataa kusikia ujumbe wa Mungu.

Mfalme Sedekia alikaidi mambo ya Babeli. Kwa hivyo Mfalme Nebukadreza alikuja na kuzingira mji wa Yerusalemu.

Mungu alipea Yeremia ujumbe mwingine, “Msipomtii Mungu, Mfalme wa Babeli atamchukua.” Makuhani na wakuu walikasirika sana. Walitupa Yeremia ndani ya kisima. Maji kwa kisima yalikuwa yamekauka lakini chini yake kulikuwa na matope nyingi ya gamu. Yeremia aliingia ndani ya matope. Hangeweza kujitoa mwenyewe. Yeremia aliachwa ndani ya kisima ili afe kwa njaa na kiu.

Kulikuwa na mtu wa imani Yerusalemu. Jina lake lilikuwa Ebedmeleki. Ebedmeleki aliende kuomba Mfalme Sedekia aokoe maisha ya Yeremia. Mfalme Sedekia alimruhusu Ebedmeleki amwokoe Yeremia.

Ebedmeleki alichukua watu waende wamsaidie. Waliteremshia Yeremia kamba. Waliteremsha pia vifurushi vya viraka na nguo kukuu. Yeremia alijifunga kamba. Alichukua hivyo viraka na kuweka kwa kwapa ili kamba isimkate. Ebedmeleki na marafiki zake walivuta Yeremia akatoka nje ya hayo matope. Walimwokoa kutoka kwa kisima.

Wababeli walizingira Yerusalemu kwa muda wa miezi kumi na minane. Baadaye walipigana na kuchukua mji wa Yerusalemu. Walitumia magogo kuvunja kuta za Yerusalemu na kuingia mjini. Waliichoma na kuiharibu. Walichukua vitu vya thamani kutoka kwa Hekalu. Watu wengi waliuawa. Watu wengi walichukuliwa mateka mpaka Babeli.

Mfalme Sedekia alijaribu kutoroka kwa giza. Yeye pamoja na familia yake walitorokea bustani kupitia kwa lango ndogo katikati ya kuta mbili. Lakini Wababeli waliwapata. Wana wa Sedekia waliuawa mbele yake. Mfalme Sedekia alipofushwa macho na kupelekwa Babeli kwa minyororo. Alijuta kwa kutosikia ujumbe wa Mungu kupitia kwa Yeremia.

Mfalme Nebukadreza alikuwa amesikia juu ya nabii Yeremia. Alisikia kwamba Yeremia alikuwa ameambia Sedekia atii Wababeli. Mfalme Nebukadreza alipeana amri ya kipekee kwamba lazima Yeremia asiumizwe. Yeremia alikupaliwa kuishi kwa nchi yake. Ebedmeleki naye alibaki kwa nchi yake kwa sababu alikuwa ameokoa Yeremia.